

TUMSIFU BWANA!



Kimeandaliwa na Watson Goodman

Bure – Kisiuzwe

TUMSIFU BWANA!

Bwana amenipa changamoto kutumia dakika 15 kila siku za kumsifu Yeye. Nikagundua kuwa hili hunifanya niwe Mkristo mwenye furaha na mshindi zaidi.

Tafadhalii usisome kijitabu hiki hivi hivi tu. Kitumie kuku-ongoza katika undani mkubwa, bubujiko la moyo wa kumsifu aliye wa ajabu, Mungu wetu aishiye. Chagua sehemu za Maandiko hizi kila asubuhi na kaa katika kusifu mbele za Bwana. Hebu sifa kwake iwe ya kuendelea, tabia idumuyo.

Junge na Jopo la Kumsifu Dunia Nzima

Bwana amenipa changamoto ya *kuuliza watu milioni moja katika nchi zote duniani kote* kumsifu Yeye kwa dakika 15 kila siku. Hebu tupime nia zetu. Ni *nini muhimu zaidi kuliko mioyo iliyobubujika sifa kwa Mfalme wa Wafalme? Je utakuwa mmoja wa hao milioni?* –Watson Goodman (1920-2002)

Scripture text reprinted from the Bible in Kiswahili by permission of United Bible Societies Africa Regional Centre, Nairobi, Kenya.

MSIFUNI BWANA KWA FURAHA INAYOFURIKA 1

Mfurahieni BWANA; shangi-lieni, enyi wenyе haki. Pigeni vigelegele vya furaha; ninyi nyote mlio wanyofu wa moyo.

–Zaburi 32:11

Neno la Bwana likaenea katika nchi ile yote. Na wanafunzi walijaa furaha na Roho Mtakatifu. –Matendo 13:49, 52

Ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuone-kane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika

kufunuliwa kwake Yesu Kristo. Naye mwampenda, ijapokuwa hamkumwona; amba-ye ijapokuwa hamwoni sasa, mnamwamini; na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka, yenyе utukufu. –1 Petro 1:7, 8

Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho. Lakini kama mnavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe. –1 Petro 4:12, 13

2 WEKA MOYO WAKO KATIKA KUMSIFU BWANA

“Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote.”

–Kumbukumbu la Torati 6:5

Nitamshukuru Bwana kwa moyo wangu wote; nitayasi-mulia matendo yako yote ya ajabu.

–Zaburi 9:1

Nitakushukuru kwa moyo wangu wote, mbele ya miungu nitakuimbia zaburi. Nitasujudu nikilikabili hekalu lako takatifu, nitalishukuru jina lako, kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu wako, kwa

maana umeikuza ahadi yako, kuliko jina lako lote.

–Zaburi 138:1, 2

Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana. Naam, vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi jina lake takatifu.

–Zaburi 103:1

“Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema.”

–Luka 6:45a

Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu.

–Waefeso 5:19

MATUNDA YA KUSIFU

3

*Mungu Hukaa Palipo
Na Kusifu*

Na Wewe U Mtakatifu, uke-
tiye juu ya sifa za Israeli.

-Zaburi 22:3

*Ili Kuwa na Furaha na
Matunda Weka Sifa
Zikae Mbele za Mungu*

Ee Mungu, sifa zakulaiki ka-
tika Sayuni. -Zaburi 65:1a

Njoni, tumwimbie BWANA, tu-
mfanyie shangwe mwamba
wa wokovu wetu. Tuje mbele
zake kwa shukrani, tumfa-
nyie shangwe kwa zaburi.

-Zaburi 95:1, 2

Watu na wakushukuru, Ee
Mungu, watu wote na waku-
shukuru. Nchi imetoa mazao
yake; MUNGU, Mungu wetu,
ametubariki. -Zaburi 67:5, 6

Kusifu Huponya Woga

Maana Mungu hakutupa ro-
ho ya woga, bali ya nguvu
na ya upendo na ya moyo wa
kiasi. -2 Timotheo 1:7

*Kusifu Ni Dhabihu ya Mkristo;
Jitoe Mwenyewe kwa Hilo*

Basi, kwa njia yake yeye, na
tumpe Mungu dhabihu ya si-
fa daima, yaani, tunda la mi-
domo iliungamayo jina lake.

-Waebriana 13:15

MBINGU IMEJAZWA KWA KUSIFU

Haleluya. Msifuni BWANA kutoka mbinguni; msifuni kati-ka mahali palipo juu. Msifuni, enyi malaika zake wote; msifuni, majeshi yake yote. Msifuni, jua na mwezi; msifuni, nyota zote zenye mwanga. Msifuni, enyi mbingu za mbi-ngu, nanyi maji mlioko juu ya mbingu. Na vilisifu jina la BWANA, kwa maana aliamuru, vikaumbwa. Amevithibitisha hata milele na milele, ametoa amri wala haitapita. Na walisi-
fu jina la BWANA, maana jina lake peke yake limetukuka; adhama yake i juu ya nchi na mbingu. –Zaburi 148:1-6, 13

*Weka katika Zoezi Sasa Ikiwa
Unaelekea Upande Ule*

Mbingu na nchi zimsifu, ba-hari na vyote viendavyo nda-ni yake. –Zaburi 69:34

*Ndiyo Sababu Wewe
Umeokolewa*

Basi, heshima hii ni kwenu ninyi mnaoamini. Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake ye-ye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu; ninyi mliokuwa kwa-nza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu. –1 Petro 2:7a, 9, 10a

KILA MMOJA ANAALIKWA KATIKA KWAYA YAKE YA KUSIFU

5

Enyi watu wote, pige ni ma-kofi, mpigieni Mungu kelele kwa sauti ya shangwe. Mwi-mbieni Mungu, naam, imbe-ni; mwimbieni mfalme wetu, naam, imbeni. Maana Mungu ndiye mfalme wa dunia yote.
–Zaburi 47:1, 6, 7a

“Mpigie Mungu kelele za shangwe, nchi yote, nchi yote itakusujudia na kukuimbia, naam, italiimbia jina lako.”
–Zaburi 66:1, 4

Mataifa na washangilie, naam, waimbe kwa furaha, maana kwa haki utawahukumu watu,

na kuwaongoza mataifa walio-ko duniani. –Zaburi 67:4

Kila mwenye pumzi na amsifu BWANA. Haleluya.
–Zaburi 150:6

Haleluya. Enyi mataifa yote, msifuni BWANA, enyi watu wote, mhimidini. Maana fa-dhili zake kwetu sisi ni kuu, na uaminifu wa BWANA ni wa milele. –Zaburi 117:1, 2

Kwa kuwa neno la BWANA lina adili, na kazi yake yote huitenda kwa uaminifu.
–Zaburi 33:4

6 MSIFUNI BWANA KWA VILE YEYE ALIVYO

Ndipo hao watu wakafurahi, kwa sababu wametoa kwa hiari yao wenyewe, kwa sababu kwa ukamilifu wa moyo, kwa hiari yao wenyewe, wamemtolea BWANA; mfalme Daudi naye akafurahi kwa furaha kuu. Kwa hiyo Daudi akamhimidi BWANA, mbele ya mkutano wote; naye Daudi akasema, Uhimidiwe, Ee BWANA, Mungu wa Israeli baba yetu, milele na milele. Ee BWANA, ukuu ni wako, na uweza, na utukufu, na kushinda, na enzi; maana vitu vyote vili-vyo mbinguni na duniani ni

vyako; ufalme ni wako, Ee BWANA, nawe umetukuzwa, u mkuu juu ya vitu vyote. Utajiri na heshima hutoka kwa-ko wewe, nawe watawala juu ya vyote; na mkononi mwako mna uweza na nguvu; tena mkononi mwako mna kuwatukuza na kuwa-wezesha wote. Basi sasa, Mungu wetu, twakushukuru na kulisifu jina lako tukufu.

–1 Nyakati 29:9-13

“Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni BWANA wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake.”

–Isaya 6:3b

MSIFUNI BWANA KWA VILE YEYE ALIVYO

7

Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo ili-yochangamana na moto, na wale wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake, walikuwa wamesimama kandokando ya hiyo bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu. Nao waumiba wimbo wa Musa, mtumwa wa Mungu, na wimbo wa Mwana-Kondoo, wakisema, "Ni makuu, na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; Ni za haki, na za kweli, njia zako, Ee Mfalme wa mataifa. Ni nani asiyekucha, Ee Bwana, na kulitukuza jina lako?

kwa kuwa wewe peke yako u Mtakatifu; kwa maana mataifa yote watakuja na kusujudu mbele zako; kwa kuwa matendo yako ya haki yamekwisha kufunuliwa." -Ufunuo 15:2-4

Nakuagiza mbele za Mungu anayevihifadhi hai vitu vyote, na mbele za Kristo Yesu,... kwamba uilinde amri hii pasipo mawaa,...hata kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo; ambako yeye kwa majira yake atakudhihirisha, yeye aliyehimidiwa, Mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana.

-1 Timotheo 6:13-15

8 MSIFUNI BWANA KWA VILE YEYE ALIVYO

Na hao wenye uhai wanapompa yeye aketiye juu ya kiticha enzi utukufu, na heshima, na shukrani, yeye aliye hai hata milele na milele, ndipo hao wazee ishirini na wanne huanguka mbele zake yeye aketiye juu ya kile kiticha enzi, nao humsujudia yeye aliye hai hata milele na milele, nao huzitupa taji zao mbele ya kile kiticha enzi, wakisema, "Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa we-wewe ndiwe uliyeviumba vituvyote, na kwa sababu ya ma-

penzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa." -Ufunuo 4:9-11

Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkuutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabilia, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiticha enzi, na mbele za Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao; wakilia kwa sauti kuu wakisema, "Wokovu una Mungu wetu aketiye katikaki kiticha enzi, na Mwana-Kondoo." -Ufunuo 7:9, 10

SIFUNI UKUU WAKE USIOCHUNGUZIKA

9

BWANA ndiye mkuu mwenye kusifiwa sana, wala ukuu wake hautambulikani. Kizazi kwa kizazi kitayasifu matendo yako, kityatangaza matendo yako makuu. Nitaifikiri fahari ya utukufu wa adhama yako, na matendo yako yote ya ajabu. Watu watayataja matendo yako ya kutisha, nami nitausimulia ukuu wako. Watalihubiri kumbukumbu la wema wako mkuu. Wataiimba haki yako. BWANA ana fadhili, ni mwangi wa huruma, si mwe-pesi wa hasira, ni mwangi wa rehema, BWANA ni mwema kwa watu wote, na rehema

zake zi juu ya kazi zake zote. Ee BWANA, kazi zako zote zitakushukuru, na wacha Mungu wako watakuhimidi. Wataune-na utukufu wa ufalme wako, na kuuhadithia uweza wako. Ili kuwajulisha watu matendo yake makuu, na utukufu wa fahari ya ufalme wake. Ufalme wako ni ufalme wa zamani zote.

–Zaburi 145:3-13a

Haleluya. Msifuni Mungu katika patakatifu pake; msifuni katika anga la uweza wake. Msifuni kwa matendo yake makuu; msifuni kwa kadiri ya wingi wa ukuu wake.

– Zaburi 150:1, 2

MSIFU YEYE KWA KITI CHAKE CHA ENZI NA UWEZO

**Kiti chako cha enzi, Mungu,
ni cha milele na milele.**

–Zaburi 45:6a

BWANA asema hivi, “Mbingu ni kiti changu cha enzi, na dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu; mtanijengea.”

–Isaya 66:1a

BWANA ameweeka kiti chake cha enzi mbinguni, na ufalme wake unavitawala vitu vyote. Mhimidini BWANA, enyi malaika zake, ninyi mlion ho-dari, mtendao neno lake, mkiisikiliza sauti ya neno lake. Mhimidini BWANA, enyi majeshi yake yote, ninyi wa-

tumishi wake mfanyao ma-penzi yake. Mhimidini BWA-NA, enyi matendo yake yote, mahali pote pa milki yake. Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA.

–Zaburi 103:19-22

Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapaku-onekana.

–Ufunuo 20:11

Yesu akawakazia macho, aka-waambia, “Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezeekana.”

–Mathayo 19:26

Na kuonekana kwake ule utukufu wa BWANA kulikuwa kama moto uteketezao, juu ya mlima machoni pa wana wa Israeli. -Kutoka 24:17

Na ahimidiwe BWANA, Mungu, Mungu wa Israeli, atendaye miujiza Yeye peke yake; jina lake tukufu na lihimidiwe milele; dunia yote na ijae utukufu wake. Amina na Amina. -Zaburi 72:18, 19

Ingia ndani ya jabali; ukajifiche mavumbini mbele za utisho wa BWANA, mbele za utukufu wa enzi yake. Macho ya mwanadamu yaliyoinuka

yatashushwa chini, na kiburi cha mwanadamu kitainamishwa, naye BWANA, yeze peke yake, atatukuzwa siku hiyo.

-Isaya 2:10, 11

“Na utukufu wa BWANA utafunuliwa, na wote wenye mwili watauona pamoja; kwa kuwa kinywa cha BWANA kime-nena haya.” -Isaya 40:5

“Jua halitakuwa nuru yako tena wakati wa mchana, wala mwezi hautakupa nuru kwa mwangaza wake; bali BWANA atakuwa nuru ya milele kwa-ko, na Mungu wako atakuwa utukufu wako.” -Isaya 60:19

Yote kwa Kristo Huishi Milele
 Maana kwa kuwa mauti ili-
 letwa na mtu, kadhalika na
 kiyama ya wafu ililetwa na
 mtu. Kwa kuwa kama katika
 Adamu wote wanakufa, ka-
 dhalika na katika Kristo wote
 watahuishwa. Lakini kila
 mmoja mahali pake; limbuko
 ni Kristo; baadaye walio wa-
 ke Kristo, atakapokuja. Hapo
 ndipo mwisho, atakapompa
 Mungu Baba ufalme wake;
 atakapobatilisha utawala wote,
 na mamlaka yote, na nguvu.
 Maana sharti amiliki yeye,
 hata awaweke maadui wake
 wote chini ya miguu yake.

Adui wa mwisho atakayeba-
 tilishwa ni mauti.

–1 Wakorintho 15:21-26

***Humtupa Nje Shetani
 siku ya Mwisho***

“Sasa hukumu ya ulimwe-
 ngu huu ipo; sasa mkuu wa
 ulimwengu huu atatupwa nje.”

–Yohana 12:31

Na yule Ibilisi, mwenye ku-
 wadanganya, akatupwa kati-
 ka ziwa la moto na kiberiti,
 alimo yule mnyama na yule
 nabii wa uongo. Nao watate-
 swa mchana na usiku hata mi-
 lele na milele. –Ufunuo 20:10

MSIFUNI YEYE KWA ENZI YAKE KUU

13

Wajue ya kuwa Wewe, uitwaye jina lako YEHODA, ndiwe peke yako Uliye juu, juu ya nchi yote. -Zaburi 83:18

“BWANA huua, naye hufanya kuwa hai; hushusha hata kuzimu, tena huleta juu. BWANA hufukarisha mtu, naye hutajirisha; hushusha chini, tena huinua juu. Humwinua mnyonge kutoka mavumbini, humpandisha mhitaji kutoka jaani, ili awaketishe pamoja na wakuu, wakakirithi kiti cha enzi cha utukufu; kwa maana nguzo za dunia zina BWANA, naye ameuweka ulimwengu juu yake.” -1 Samweli 2:6-8

Maana Wewe, BWANA, ndiwe Uliye juu, juu sana kuliko nchi yote; umetukuka sana juu ya miungu yote.

-Zaburi 97:9

Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina. -Wafilipi 2:9

BWANA ametamalaki, amejivika adhama, BWANA amejivika, na kujikaza nguvu. Naam, ulimwengu umethibitika usitikisike; kiti chako kimekuwa thabiti tokea zamani; Wewe ndiwe uliye tangu milele.

-Zaburi 93:1, 2

MUNGU WETU MKUU AMETUKUKA

Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu, nitakuzwa katika mataifa, nitakuzwa katika nchi.

–Zaburi 46:10

BWANA ni mkuu juu ya mataifa yote, na utukufu wake ni juu ya mbingu. –Zaburi 113:4

Ee BWANA, utukuzwe kwa nguvu zako, nasi tutaimba na kuuhimidi uweza wako.

–Zaburi 21:13

Mtukuzeni BWANA, Mungu wetu; sujuduni penye kitikitaa miguu yake; ndiye mtakatifu.

–Zaburi 99:5

BWANA ametukuka; kwa manaa anakaa juu; amejaza

Sayuni hukumu na haki.

–Isaya 33:5

Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; amba ye jina lake ni Mtakatifu; asema hivi; “Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu; tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kuyenyekoa, ili kuzifufua roho za wanyenyekova, na kuifufua mioyo yao waliotubu.”

–Isaya 57:15

Bali BWANA wa majeshi ametukuzwa katika hukumu, na Mungu aliye Mtakatifu ametakaswa katika haki.

–Isaya 5:16

“Sasa basi ikiwa mtaitii suti yangu kweli kweli, na kuhlishika agano langu, hapo ndipo mtakapokuwa tunu kwantru; maana dunia yote piani mali yangu.” –Kutoka 19:5

“Nayo nchi haitauzwa kabisa kabisa; kwani nchi ni yangu mimi.”

–Mambo ya Walawi 25:23a

Maana vitu vyote vilivyo mbinguni na duniani ni vyako; ufalme ni wako, Ee BWANA, na we umetukuzwa, u mkuu juu ya vitu vyote. Lakini mimi ni nani, na watu wangu ni nani, hata tuweze kutoa kwa hiari

hivi? kwani vitu vyote vyatoka kwako, na katika vitu vyako mwenyewe tumekutolea.

–1 Mambo ya Nyakati 29:11b, 14

Aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, aka-mweka mkono wake wa kuumbe katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo.

–Waefeso 1:20-22

16 MSIFUNI YEYE KWA KWAKE NI BWANA

Ezra akasema, Wewe ndiwe BWANA, wewe peke yako; wewe ulifanya mbingu, mbingu za mbingu, pamoja na jeshi lake lote, dunia na vyote vilivyomo, bahari na vitu vyote vilivyomo, nawe unavihifadhi vitu hivi vyote; na jeshi la mbinguni lakusujudu wewe.

—Nehemia 9:6

Nitakusifu Wewe, Bwana, Mungu wangu, kwa moyo wangu wote, Nitalitukuza jina lako milele. —Zaburi 86:12

Lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake,

nasi tunaishi kwake; yuko na Bwana mmoja Yesu Kristo, ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo, na sisi kwa yeye huyo. —1 Wakorintho 8:6

Mimi ni BWANA; ndilo jina langu; na utukufu wangu sitampa mwingine, wala sitawapa sanamu sifa zangu. —Isaya 42:8

“Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo.” —Matendo 2:36

Ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba. —Wafilipi 2:11b

MTUKUZE MUNGU KATIKA KUSIFU

17

“Atoaye dhabihu za kushukuru, ndiye anayenitukuza. Naye autengenezaye mweneendo wake, nitamwonyesha wokovu wa Mungu.” –Zaburi 50:23

Nitalisifu jina la Mungu kwa wimbo, nami nitamtukuza kwa shukrani. –Zaburi 69:30

Ndiwe Mungu wangu, nami nitakushukuru, ndiwe Mungu wangu, nami nitakutukuza.

–Zaburi 118:28

Ili kwa moyo mmoja na kwa kinywa kimoja mpate kumtukaza Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo.

–Warumi 15:6

Mpeni BWANA utukufu wa jina lake; mwabuduni BWANA kwa uzuri wa utakatifu.

–Zaburi 29:2

Ninyi mnaomcha BWANA, msi-funi, enyi nyote mlion wazao wa Yakobo, mtukuzeni, mcheni, enyi nyote mlion wazao wa Israeli.

–Zaburi 22:23

Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katiaka mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina.

–1 Petro 4:11

HUBIRI UTUKUFU WAKE NA UKUU

Wahubirini mataifa habari za utukufu wake, na watu wote habari za maajabu yake. Kwa kuwa BWANA ni mkuu mwenye kusifiwa sana. Na wa kuhofiwa kuliko miungu yote.

—Zaburi 96:3, 4

Ee Mungu, utukuzwe juu ya mbingu, na juu ya nchi yote uwe utukufu wako.

—Zaburi 57:5

Imbeni utukufu wa jina lake, tukuzeni sifa zake.

—Zaburi 66:2

“Ee BWANA Mungu, umeanza kumwonyesha mtumishi wako ukubwa wako, na mkono

wako wa nguvu; kwani kuna mungu gani mbinguni au duniani awezaye kufanya mfano wa kazi zako, na mfano wa matendo yako yenye nguvu?”

—Kumbukumbu la Torati 3:24

Mpigieni BWANA vigelegele, enyi wenye haki, kusifu kunawapasa wanyofu wa moyo.

—Zaburi 33:1

Katika BWANA nafsi yangu itajisifu, wanyenyekevu wasikie wakafurahi.

—Zaburi 34:2

Ee Mungu, moyo wangu u thabiti, nitaimba, nitaimba zaburi, naam, kwa utukufu wangu.

—Zaburi 108:1

MSIFU MUNGU KWA MAKUSUDI YAKE MAKUU 19

Ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho; kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu. -Waefeso 3:10, 11

Atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi. -1 Yohana 3:8

Na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukicha-

guliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, amba ye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake.

-Waefeso 1:11

Ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele, na sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake Mwokozi wetu Kristo Yesu.

-2 Timotheo 1:9, 10a

MSIFUNI MUNGU KWA KAZI ZAKE KUU

Nikiziangalia mbingu zako,
kazi ya vidole vyako, mwezi
na nyota ulizoziratibisha; mtu
ni kitu gani hata umkumbu-
ke, na binadamu hata umwa-
ngalie? -Zaburi 8:3, 4

Mbingu zauhubiri utukufu
wa Mungu, na anga laitanga-
za kazi ya mikono yake.

-Zaburi 19:1

Ili niitangaze sauti ya ku-
shukuru, na kuzisimulia kazi
zako za ajabu. -Zaburi 26:7

Ee BWANA, Mungu wangu,
umefanya kwa wingi miujiza
yako na mawazo yako kwetu;

hakuna awezaye kufanani-
shwa nawe; kama ningepe-
nda kuyatangaza na kuyahu-
biri, ni mengi sana hayahe-
sabiki. -Zaburi 40:5

Nitakushukuru kwa kuwa
nimeumbwa kwa jinsi ya aja-
bu ya kutisha. Matendo yako
ni ya ajabu, na nafsi yangu
yajua sana. -Zaburi 139:14

Matendo ya BWANA ni makuu,
yafikiriwa sana na wape-
ndezwao nayo. Kazi yake ni
heshima na adhama, na haki
yake yakaa milele.

-Zaburi 111:2, 3

MSIFUNI YEYE KWA MAPENZI NA NJIA ZAKE 21

Kwa Mapenzi Yake Makuu

Wala si kwa utumwa wa macho tu kama wajipendekezao kwa wanadamu; bali kama watumwa wa Kristo, mkitenda yampendezayo Mungu kwa moyo.

—Waefeso 6:6

Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu. —Yohana 7:17a

Kwa maana ye yote ataka-yeafanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni, huyu ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu.

—Matayo 12:50

Kwa Njia Zake Kuu

Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani!

—Warumi 11:33

Mungu, njia yake ni kamili-fu, ahadi ya BWANA imehaki-kishwa.

—Zaburi 18:30a

Kwa maana kama vile mbi-ngu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu.

—Isaya 55:9a

“...Mfalme wa mbinguni, namtukuza na kumheshimu; maana matendo yake yote ni kweli.”

—Danieli 4:37a

MSIFUNI YEYE KWA JINA LAKE TUKUFU

Kama lilivyo jina lako, Ee Mungu, ndivyo na sifa yako hata miisho ya dunia. Mpeni BWANA utukufu wa jina lake, leteni sadaka mkaziingie nyua zake. Mwabuduni BWANA kwa uzuri wa utakatifu, tetemekeni mbele zake, nchi yote. –Zaburi 48:10a; 96:8, 9

Na katika siku hiyo mtasema, “Mshukuruni BWANA, liitiensi jina lake; yatangazeni matendo yake kati ya mataifa, litajeni jina lake kuwa li-metukuka.” –Isaya 12:4

“Kama hutaki kutunza kufanya maneno yote ya torati

hii yaliyoandikwa katika kitabu hiki, upate kulicha jina hili la fahari na utisho, BWANA, MUNGU WAKO; ndipo atakapofanya BWANA mapigo yako yawe ya ajabu, na mapigo ya uzao wako, mapigo makubwa kwa kweli, ya kudumu sana, na magonjwa mazito ya kudumu sana.” –Kum. 28:58, 59

Akafanya hayo siku nyingi. Lakini Paulo akasikitika, aka-geuka akamwambia yule pepo, “Nakuamuru kwa jina la Yesu Kristo, mtoke huyu. Akamtoka saa ile ile.”

–Matendo 16:18

Tumejisifia Mungu mchana kutwa, na jina lako tatalishukuru milele. –Zaburi 44:8

BWANA akashuka ndani ya lile wingu, akasimama pamoja naye huko, akalitangaza jina la BWANA. –Kutoka 34:5

“Mkamhimidi BWANA, Mungu wenu, tangu milele na hata milele. Na lihimidiwe jina lako tukufu, lililotukuka kuliko baraka zote na sifa zote.” –Nehemia 9:5b

Na vilisifu jina la BWANA, kwa maana aliamuru, vikau-mbwa. Na walisifu jina la BWANA, maana jina lake peke

yake limetukuka; adhama yake i juu ya nchi na mbingu.

–Zaburi 148:5, 13

Kwa ukunjufu wa moyo nitakutolea dhabihu; Ee BWANA, nitalishukuru jina lako, maana ni jema. –Zaburi 54:6

Nanyi mtakula chakula tele na kushiba, na kulihimidi jina la BWANA, Mungu wenu, ali-yewatendea mambo ya ajabu; na watu wangu hawatatahayari kamwe. –Yoeli 2:26

Nitalisifu jina la Mungu kwa wimbo, nami nitamtukuza kwa shukrani. –Zaburi 69:30

Nitamshukuru BWANA kwa kadiri ya haki yake; nitalii-mbia jina la BWANA Aliye juu.

—Zaburi 7:17

“Tazama, bikira atachukua mimba, Naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake Imanueli;” Yaani, “Mungu pamoja nasi.” —Mathayo 1:23

Wewe, MUNGU, Bwana wetu, jinsi lilivyo tukufu jina lako duniani mwote! —Zaburi 8:9

Kwa hiyo tena Mungu ali-mwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbi-

nguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi. —Wafilipi 2:9, 10

Mtukuzeni BWANA pamoja nami, na tuliadhimishe jina lake pamoja. —Zaburi 34:3

Na walishukuru jina lake kuu la kuhofiwa; ndiye mta-katifu. —Zaburi 99:3

Jina la BWANA lihimidiwe tangu leo na hata milele. Toka maawio ya jua hata machweo yake jina la BWANA hu-sifiwa. —Zaburi 113:2, 3

Mataifa yote walinizunguka; kwa jina la BWANA naliwakatilia mbali. —Zaburi 118:10

BAADHI YA MAJINA NA VYEO VYA KRISTO 25

- Uwezo wa Enzi Yake***
Alfa na Omega–Mwenyezi
–Ufunuo 1:8
- Mbarikiwa na Aliyehimidiwa pekee**—1 Timotheo 6:15
- Kristo ni Bwana**—Luka 2:11
- Kristo ni uwezo wa Mungu na hekima ya Mungu**
—1 Wakorintho 1:24
- Mungu**—Yohana 1:1
- Mungu wa dunia yote**
—Isaya 54:5
- Kichwa cha enzi yote na mamlaka**—Wakolosai 2:10
- MIMI NIKO**—Yohana 8:58
- Immanueli (Mungu pamoja nasi)**
—Mathayo 1:23

- Mhukumu wa walio hai na wafu**—Matendo 10:42
- Mfalme wa utukufu**
—Zaburi 24:7, 10
- MFALME WA WAFALME, NA BWANA WA MABWANA**
—Ufunuo 19:16
- Bwana wa majeshi**
—Isaya 54:5; Zaburi 24:10
- Bwana Mungu Mwenyezi**
—Ufunuo 15:3
- Mtakatifu Sana**—Danieli 9:24
- Mtawala**—Mathayo 2:6
- Mwana wa Mungu**
—Yohana 9:35-37
- Wa ajabu, Mshauri, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani**—Isaya 9:6

26 BAADHI YA MAJINA NA VYEO VYA KRISTO

Tamaa ya Mataifa Yote

–Hagai 2:7

Shahidi Mwaminifu

–Ufunuo 1:5

Rafiki wa wenye dhambi

–Mathayo 11:19

Mfalme juu ya nchi yote

–Zekaria 14:9

Bwana wa wote

–Matendo 10:36

Mkombozi kwa ajili ya wote

–1 Timotheo 2:6

Mhukumu mwenye Haki

–2 Timotheo 4:8

**Mchungaji na Mwangalizi
wa roho zenu**–1 Petro 2:25

Mwana wa Adamu

–Mathayo 8:20

Jiwe Lililokataliwa

–Mathayo 21:42

Kama Mwokozi

Mwanzilishi wa wokovu wa

milele–Waebrania 5:9

Zawadi ya Mungu

–Yohana 4:10

Yesu Kristo Mwokozi wetu

–Tito 3:6

Masihi–Yohana 1:41

Masihi aliye Mfalme

–Danieli 9:25

Sadaka na dhabihu kwa

Mungu–Waefeso 5:2

Mkombozi–Isaya 59:20

Ufufuo na uzima

–Yohana 11:25

Mwokozi Yesu Kristo

–2 Timotheo 1:10

BAADI YA MAJINA NA VYEO VYA KRISTO

27

- Yeye Aliye kwa Waamini***
Mwombezi–1 Yohana 2:1
Mwanzilishi na mkamilishaji
wa imani yetu–Waebrania 12:2
Chipukizi la haki–Yer. 33:15
Mkate wa uzima–Yohana 6:48
Bwana Arusi–Mathayo 9:15
Jiwe kuu la pembedi–Efe. 2:20
Mchungaji Mkuu–1 Petro 5:4
Kristo wa Mungu–Luka 9:20
Mlango wa kondoo
–Yohana 10:7, 9
Uzima wa milele
–1 Yohana 5:20
Mungu na Mwokozi Yesu
Kristo–2 Petro 1:1
Kuhani Mkuu–Waebrania 3:1

- Tumaini la utukufu–Kol. 1:27
Mfalme wa watakatifu
–Ufunuo 15:3
Roho yenye kuhuisha
–1 Wakorintho 15:45
Nuru ya ulimwengu
–Yohana 8:12
BWANA WA HAKI YETU
–Yeremia 23:6
Bwana Yesu–Matendo 7:59
Mpatanishi–1 Timotheo 2:5
Mfalme na Mwokozi
–Matendo 5:31
Mfalme wa Amani–Isaya 9:6
Nabii–Luka 24:19
Mkombozi–Zaburi 19:14
Nuru ya kweli–Yohana 1:9

28 MSIFU BWANA KWA AJILI YA NENO LA MUNGU

Lenye Pumzi ya Mungu

Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundi-sho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwangoza, na kwa kuwaadibisha katika haki. –2 Timotheo 3:16

Lina Uzima wa Milele kwa Waamini

“Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwa-min Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia.” –Yohana 3:36

Nimewaandikia ninyi mambu hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi

mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu. –1 Yohana 5:13

Lakini hizi zimeandikwa; ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.

–Yohana 20:31

Lina Uwezo

“Je! neno langu si kama mo-to?” Asema BWANA; “na kama nyundo ivunjayo mawe vipande vipande?” –Yeremia 23:29

Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye.

–Warumi 1:16a

MSIFU BWANA KWA AJILI YA NENO LA MUNGU 29

Ni Safi

Kila neno la Mungu limeha-kikishwa. –Mithali 30:5a

Maneno ya BWANA ni maneno safi. –Zaburi 12:6a

Ni kamilifu

Sheria ya BWANA ni kamilifu, huiburudisha nafsi. Ushuhuda wa BWANA ni amini, humtia mjinga hekima. –Zaburi 19:7

Lina Ukweli wa Hakika

“Kwa maana, amin, nawaa-mbia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yati-mie.” –Mathayo 5:18

Ni Kanuni Yetu ya Ukweli

Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu;... amejaanee-ma na kweli. –Yohana 1:14

Yesu akamwambia, “Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.” –Yohana 14:6

“Majani yakauka, ua lanya-uka; bali neno la Mungu wetu litasimama milele.” –Isaya 40:8

Ni Nuru Yetu

Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu. –Zaburi 119:105

30 MSIFU BWANA KWA AJILI YA NENO LA MUNGU

Limejaa Makusudi

Kwa kuwa yote yaliyotanguilia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini.

—Warumi 15:4

Linapendwa na Watu wa Mungu

Neno lako limesafika sana, kwa hiyo mtumishi wako amelipenda. —Zaburi 119:140

Ni Chakula Chetu

“Apate kukujulisha ya kuwa mwanadamu haishi kwa makte tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana.”

—Kumbukumbu la Torati 8:3b

Kama watoto wachanga wailiozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu.

—1 Petro 2:2

Ni Silaha

Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.

—Waebriania 4:12

KWA AJILI YA DAMU YAKE YA AGANO

31

Soma Kutoka 24:6-8 na
Waebrania 9

Damu ya Kristo ya Agano Jipy

“Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondleo la dhambi.” –Mathayo 26:28

Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, “Kikombe hiki ni agano jipy katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.”

–1 Wakorintho 11:25

Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu

ya agano aliyatakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema? –Waebrania 10:29

Basi, Mungu wa amani aliye-mleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji Mkuu wa kondoo, kwa damu ya agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu.

–Waebrania 13:20

Aulaye mwili wangu na kui-nywa damu yangu anao uzi-ma wa milele. –Yohana 6:54a

Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa. –Ufunuo 12:11

MSIFUNI BWANA!

Mungu Wangu Alinifia

Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliu-toa uhai wake kwa ajili yetu.

–1 Yohana 3:16a

Yeye ni Mwenyezi Aliyefufuliwa

Yesu akamwambia, “Mimi ndimi huo ufulufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapo-kufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je! unayasadiki hayo?”

–Yohana 11:25, 26

Aliununua Ukombozi Wangu

“Jitunzeni nafsi zenu, na

lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.”

–Matendo 20:28

Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iha-ribikayo, bali kwa ile isiyo-haribika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele.

–1 Petro 1:23

Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. –Warumi 8:1

MSIFUNI BWANA!

33

Nanyi mnajua ya kuwa yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani yake. –1 Yohana 3:5

“Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wa msujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipo-keaye chapa ya jina lake.”

–Ufunuo 14:11

Nasi twajua kwamba Mwana wa Mungu amekwisha kuja, naye ametupa akili kwamba tumjue yeye aliye wa kweli, nasi tumo ndani yake yeye

aliye wa kweli, yaani, ndani ya Mwana wake Yesu Kristo. Huyu ndiye Mungu wa kweli, na uzima wa milele.

–1 Yohana 5:20

“Kondoo wangu waisikia sau-ti yangu; nami nawajua, nao wanifuata. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mko-no wangu.” –Yohana 10:27, 28

“Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.”

–Yohana 17:3

MSIFUNI BWANA!

Kwa Wito wa Kutubu

Yesu aliposikia aliwaambia, Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi. –Marko 2:17

***Kwa Wokovu katika Imani
kwa Yesu***

“Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.”

–Matendo 16:31

***Kwa Kuondoa Uchungu
Kutoka Mauti***

“Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako?” Uchu-

ngu wa mauti ni dhambi, na nguvu za dhambi ni torati. Lakini Mungu na ashukuri-we atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.

–1 Wakorintho 15:55-57

Kwa Njia Pekee ya Wokovu

Yesu...akamwambia,... “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezি kuuona ufalme wa Mungu.” –Yohana 3:3

BWANA ni nguvu zangu, na wimbo wangu; naye ameku-wa wokovu wangu. Yeye ni Mungu wangu, nami nitamsifu; ni Mungu wa baba yangu, nami nitamtukuza. –Kutoka 15:2

MSIFUNI BWANA!

35

Kwa Ushirika na Kristo

Hilo tulitoliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili na-nnyi pia mpate kushirikiana nasi: na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo.

–1 Yohana 1:3

“Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlangano, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.” –Ufunuo 3:20

“Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo

hapo katikati yao.”

–Mathayo 18:20

Mungu ni mwaminifu amba-ye mliitwa na yeye mwingie katika ushirika wa Mwanawe, Yesu Kristo Bwana wetu.

–1 Wakorintho 1:9

“Siku ile ninyi mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu.” –Yohana 14:20

Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye, naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa. –1 Yohana 3:24

Msifu Yeye Zaidi na Zaidi

Nami nitatumaini daima, nitazidi kuongeza sifa zako zote. Kinywa changu kitasimulia haki na wokovu wako. Na haki yako, Ee Mungu, imefika juu sana. Wewe uliyefanya mambo makuu; Ee Mungu, ni nani aliye kama Wewe?

–Zaburi 71:14, 15a, 19

Enyi mataifa, mtukuzeni Mungu wetu, itangazeni sauti ya sifa zake.

–Zaburi 66:8

“Hayo nimewaambieni mpatte kuwa na amani ndani yantru. Ulimwenguni mnayo dhi-ki; lakini jipeni moyo; mimi

nimeushinda ulimwengu.”

–Yohana 16:33

Ujasiri Kwa Damu ya Yesu

Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia pataktifu kwa damu ya Yesu, njia ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pa-zia, yaani, mwili wake.

–Waebrania 10:19, 20

Ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwe-nyewe, wale walio na juhudini katika matendo mema.

–Tito 2:14

BWANA NI SIFA YANGU

37

Uniponye, Ee BWANA, nami nitaponyeka; uniokoe, nami nitaokoka; kwa maana wewe ndiwe uliye sifa zangu.

-Yeremia 17:14

Tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu.

-Tito 2:13

Yeye Ni Uzima Wangu wa Milele

“Kama vile ulivyompa mamlaka juu ya wote wenye mwili, ili kwamba wote uliompa awape uzima wa milele.”

-Yohana 17:2

Hali mmejazwa matunda ya haki, kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu.

-Wafilipi 1:11

Lakini wakuu wa makuhani na waandishi walipoyaona maajabu aliyoyafanya, na watoto waliopaza sauti zao hekaluni, wakisema, “Hosana, Mwana wa Daudi!” walikasirika, wakamwambia, “Wasikia hawa wasemavyo?” Yesu aka-wambia, Naam; hamkupata kusoma, “Kwa vinywa vya watoto wachanga na wanyonyao umekamilisha sifa?”

-Mathayo 21:15-16

38 MSIFU YEYE KATIKA KUJARIBIWA IMANI YAKO

Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayarri kufunuliwa wakati wa mwisho. Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali.

–1 Petro 1:5, 6

Kama wenyе huzuni, bali sikuzote wenyе furaha; kama maskini, bali tukitajirisha wengi; kama wasio na kit bali tu wenyе vitu vyote.

–2 Wakorintho 6:10

Nao wakatoka katika ile baraza, wakifurahi kwa sababu

wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo. –Matendo 5:41

Na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye. –Warumi 8:17

Ndugu, watwaeni manabii walionena kwa jina la Bwana, wawe mfano wa kustahimili mabaya, na wa uvumilivu. Angalieni, twawaita heri wao waliosubiri. –Yakobo 5:10, 11a

Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu.

–2 Wakorintho 4:17a

KABILIANA NA KILA KITU KWA KUTOA SHUKRANI 39

Bali mjazwe Roho; na kumshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo. –Waefeso 5:18b, 20

Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mki-mshukuru Mungu Baba kwa yeze. –Wakolosai 3:17

Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zifulikane na Mungu.

–Wafilipi 4:6

“Mtolee Mungu dhabihu za kushukuru; mtimizie Aliye juu nadhiri zako. Ukaniite siku ya mateso; nitakuokoa, na wewe utanitukuza.”

–Zaburi 50:14, 15

Ni Mapenzi ya Mungu

Shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu. –1 Wathesalonike 5:18

Ni Njia ya Kumkaribia Mungu

Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; nyuani mwake kwa kusifu; mshukuruni, lihimidini jina lake.

–Zaburi 100:4

Wanahesabiwa haki bure
kwa neema yake, kwa njia ya
ukombozi ulio katika Kristo
Yesu. -Warumi 3:24

Katika yeye huyo, kwa damu
yake, tunao ukombozi wetu,
masamaha ya dhambi, sawa-
sawa na wingi wa neema
yake. -Waefeso 1:7

Ili kwamba, kama vile dha-
mbi ilivyotawala katika mau-
ti, vivyo hivyo kwa njia ya
haki neema itawale hata uzi-
ma wa milele kwa Yesu Kristo
Bwana wetu. -Warumi 5:21

Ili tukihesabiwa haki kwa
neema yake, tupate kufanywa

warithi wa uzima wa milele,
kama lilivyo tumaini letu.

-Tito 3:7

Kwa Uhuru Kutoka Shetani

“Uwafumbue macho yao, na
kuwageuza waiache giza na
kuielekea nuru, waziache na
nguvu za Shetani na kumwe-
lekea Mungu; kisha wapate
msamaha wa dhambi zao, na
urithi mionganini mwao walio-
takaswa kwa imani iliyo kwa-
ngu mimi.” -Matendo 26:18

Basi mtiini Mungu. Mpinge-
ni Shetani, naye atawaki-
mbia. -Yakobo 4:7

*Sisi Ni Marafiki wa
Mungu Mwenyezi*

“Ninyi mmekuwa rafiki za-
ngu, mkitenda niwaamuruyo.”

—Yohana 15:14

Sisi Ni Wana wa Mungu

Kwa kuwa wote wanaoongo-
zwa na Roho wa Mungu, hao
ndio wana wa Mungu.

—Warumi 8:14

Sisi Ni Mabalozi wa Kristo

Basi tu wajumbe kwa ajili ya
Kristo, kana kwamba Mungu
anasihi kwa vinywa vyetu.

—2 Wakorintho 5:20a

Na kutufanya kuwa ufalme,
na makuhani kwa Mungu,
naye ni Baba yake; utukufu
na ukuu una Yeye hata milele
na milele. Amina. —Ufunuo 1:6

*Sisi Ni Viungo vya
Mwili wa Kristo*

Kwa kuwa tu viungo vya
mwili wake. —Waefeso 5:30

*Kuwa Mke kwa Mwana
Kondoo wa Mungu*

“Kwa kuwa arusi ya Mwa-
na-Kondoo imekuja, na mke-
we amejiweka tayari.” “Heri
walioalikwa karamu ya arusi
ya Mwana-Kondoo.”

—Ufunuo 19:7b, 9b

42 KUSIFU – NI SEHEMU YA IBADA YA PAMOJA

Nitakushukuru katika kusanyiko kubwa; nitakusifu kati ya watu wengi. –Zaburi 35:18

Na wamshukuru BWANA kwa fadhili zake, na maajabu yake kwa wanadamu. Na wamtukuze katika kusanyiko la watu. –Zaburi 107:31, 32a

Painulieni patakatifu mikono yenu, na kumhimidi BWANA.
–Zaburi 134:2

Maana ni nani katika mbingu awezaye kulinganishwa na BWANA? Ni nani afananaye na BWANA mionganoni mwa malaika? Mungu huogopwa sana barazani pa watakatifu, ni wa

kuhofiwa kuliko wote wanaomzunguka. –Zaburi 89:6, 7

Haleluya. Mwimbieni BWANA wimbo mpya, sifa zake katika kusanyiko la watauwa.

–Zaburi 149:1

Nitamshukuru BWANA kwa kinywa changu, naam, nita-msifu katikati ya mkutano.

–Zaburi 109:30

Haleluya. Lisifuni jina la BWANA, enyi watumishi wa BWANA, sifuni. Ninyi msimamao nyumbani mwa BWANA, nyuani mwa nyumba ya Mungu wetu.

–Zaburi 135:1, 2

Nami nimezitumainia fadhi-li zako; moyo wangu na uufurahie wokovu wako. Naam, nimwimbie BWANA, kwa kuwa amenitendea kwa ukarimu. Akatia wimbo mpya kinywani mwangu, ndio sifa zake Mungu wetu. Wengi wataona na kuogopa, nao watatumaini BWANA. –Zaburi 13:5, 6; 40:3

Mwimbieni BWANA akaaye Sayuni, yatangazeni kati ya watu matendo yake. –Zaburi 9:11

Mfanyieni BWANA shangwe, dunia yote; mtumikieni BWANA kwa furaha; njoni mbele zake kwa kuimba. –Zaburi 100:1, 2

Nitalisifu jina la Mungu kwa wimbo, nami nitamtukuza kwa shukrani. –Zaburi 69:30

Basi, BWANA, nitakushukuru kati ya mataifa, nami nitaliimbia jina lako. –Zaburi 18:49

Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine wali-kuwa wakiwasikiliza. Ghafula pakawa tetemeko kuu la nchi, hata misingi ya gereza ikatisika, na mara hiyo milango ikafunguka, vifungo vyaa wote vikalegezwa.

–Matendo 16:25, 26

Bwana ndiye aliye mkuu, na mwenye kusifiwa sana.

-Zaburi 48:1

Kwa kuwa BWANA ni mkuu mwenye kusifiwa sana; na wa kuhofiwa kuliko miungu yote. Maana miungu yote ya watu si kitu; lakini BWANA ndiye aliyezifanya mbingu. Heshima na adhama ziko mbele zake; nguvu na furaha zipo mahali pake.

-1 Mambo ya Nyakati 16:25-27

“Furahi sana, Ee binti Sayuni; piga kelele, Ee binti Yerusalem; tazama, mfalme wako anakuja kwako; ni mwenye

haki, naye ana wokovu.”

-Zekaria 9:9a

Mataifa yote uliowafanya watakuja; watakusujudia Wewe, Bwana, watalitukuza jina lako; kwa kuwa ndiwe uliye mkuu, Wewe ndiwe mfanya miujiza, ndiwe Mungu peke yako.

-Zaburi 86:9, 10

*Shangilia kwa namna zote
Furaha Takatifu*

Nao wote wanaokukimbilia watafurahi; watapiga daima kelele za furaha. Kwa kuwa Wewe unawahifadhi, walipendao jina lako watakulifurahia.

-Zaburi 5:11

NAWEZA KUMTUMAINI MUNGU WANGU MILELE 45

Mtumainini BWANA sikuzote,
Maana BWANA YEHVOA ni mwa-
mba wa milele. –Isaya 26:4

Mungu wa milele ndiye ma-
kazi yako, Na mikono ya mi-
lele i chini yako.

–Kumbukumbu la Torati 33:27a

Mungu kwetu sisi ni kimbilio
na nguvu, msaada utakaoone-
kana tele wakati wa mateso.
Kwa hiyo hatutaogopa ijapo-
badilika nchi, ijapotetemeka
milima moyoni mwa bahari.
Maji yake yajapovuma na
kuumka, ijapopepesuka mi-
lima kwa kiburi chake. Kuna
mto, vijito vyake vyaufurahi-

sha mji wa Mungu, patakatifu
pa maskani zake Aliye juu. Mu-
ngu yu katikati yake hauta-
tetemeshwa; Mungu atausaidia
asubuhi na mapema. Mataifa
yalighadhibika, falme zikata-
haruki; alitoa sauti yake, nchi
ikayeyuka. –Zaburi 46:1-6

“Jina lake utamwita Yesu.
Huyo atakuwa mkuu, ataitwa
Mwana wa Aliye juu, na Bwana
Mungu atampa kiti cha enzi
cha Daudi, baba yake. Ataimili-
ki nyumba ya Yakobo hata
milele, na ufalme wake utaku-
wa hauna mwisho.”

–Luka 1:31b-33

46 TUMECHAGULIWA KUMSIFU KRISTO MILELE

Yeye aliye Mungu pekee, Mwokozi wetu kwa Yesu Kristo Bwana wetu; utukufu una yeye, na ukuu, na uwezo, na nguvu, tangu milele, na sasa, na hata milele. Amina.

—Yuda 25

Kusifu Utukufu Wake

Nasi katika huyo tupate kuwa sifa ya utukufu wake, sisi tuliotangulia kumwekea Kristo tumaini letu. Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Ro-

ho yule wa ahadi aliye Matakif. Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake.

—Waefeso 1:12-14

Na hii ndiyo dua yangu, kwamba pendo lenu lizidi kuwa jingi sana, katika hekima na ufahamu wote; mpate kuyakubali yaliyo mema; ili mpate kuwa na mioyo safi, bila kosa, mpaka siku ya Kristo; hali mmejazwa matunda ya haki, kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu.

—Wafilipi 1:9-11

MSIFUNI YEYE DAIMA NA MILELE

47

Nitamhimidi Bwana kila wakati, sifa zake zi kinywani mwangu daima. –Zaburi 34:1

Na sisi tulio watu wako, na kondoo za malisho yako, tutakushukuru milele; tutazisimulia sifa zako kizazi kwa kizazi. –Zaburi 79:13

Wala hawapumziki mchana wala usiku, wakisema, “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, aliye kuwako na aliyeko na atakayekuja.” Na hao wenye uhai wanapompa ye ye aketiye juu ya kitii cha enzi utukufu, na

heshima, na shukrani, ye ye aliye hai hata milele na milele, ndipo hao wazee ishirini na wanne huanguka mbele zake ye ye aketiye juu ya kile kitii cha enzi, nao humsujudia ye ye aliye hai hata milele na milele, nao huzitupa taji zao mbele ya kile kitii cha enzi, wakisema, “Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa.” –Ufunuo 4:8b-11

48 MWABUDU KRISTO KWA SABABU AMESTAHILI

Nao waimba wimbo mpya wakisema, "Wastahili wewe kikitwaa hicho kitabu na ku-zifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulilia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabilia na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhanani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi." Ni-kaona nikasikia sauti ya ma-laika wengi pande zote za kile kititi cha enzi, na za wale wenye uhai, na za wale wazee, na hesabu yao ilikuwa elfu kumi mara elfu kumi na elfu mara elfu, wakisema kwa sauti

kuu, "Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka." Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisia, vikisema, "Baraka na he-shima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kitititi cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele." Na wale wenye uhai wan-ne wakasema, "Amina." Na wale wazee wakaanguka, waka-sujudu.

-Ufunuo 5:9-14

NGUVU ZA KIROHO KATIKA KUSIFU

Utukufu wa Bwana ulijaza nyumba ya Mungu kutokana na sifa (2 Mambo ya Nyakati 5:13, 14). Kumsifu Bwana kabla ya vita kulileta ushindi mkubwa (2 Mambo ya Nyakati 20:1-24). “Na Wewe U Mtakatifu, uketiye juu ya sifa za Israeli” (Zaburi 22:3). Mungu anakaa katika sifa za watu wake walioteuliwa. Mtu anayemsifu Mungu kwa kweli kutoka moyoni atajazwa zaidi Rohoni, kwa maana Mungu anakaa katika sifa hizo. Sifa ni njia ya hakika kuwa na uwepo na uwezo zaidi wa Mungu katika maisha ya mtu.

Nguvu za kiroho kutoka kwa Bwana huja kwa Roho wake (“mjazwe kwa Roho”); kwa Neno lake, Damu yake, Jina lake, Upendo wake; kupitia maombi ya kumaanisha, yenye moto wa mwenye haki; na kupitia utiifu kwa Mungu. Katika kijitabu hiki bado tumeona kipimo kingine cha nguvu ile ya kumsifu Bwana. Kwa kadiri mtu anavyompa Mungu sifa ya upendo, ndivyo atakavyokuwa na nguvu zaidi za kiroho.

Published in numerous languages by World Missionary Press, Inc.,
as God supplies funds in answer to prayer. **For questions or more
information by country, visit: www.wmp-contacts.org**

World Missionary Press
PO Box 120
New Paris, IN 46553-0120 USA
www.wmpress.org

1-23

1218 Kiswahili PTL